

OFISI YA RAIS
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
SHULE YA SEKONDARI BUJELA

S.L. P 347,
TUKUYU-MBEYA,
NAMBA YA SIMU: 0759-924630 /
0628-807662

Tarehe: 06 December, 2020

Kumb. Na

Jina la Mwanafunzi

S.L. P

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUJELA

WILAYA YA RUNGWE, MKOA WA MBEYA MWAKA 2021

01. UTANGULIZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari BUJELA mwaka 2021. Shule ya sekondari BUJELA ipo umbali wa km 12 mwa mji mkuu wa Tukuyu katika wilaya ya Rungwe mkoa wa Mbeya.

Muhula wa kwanza wa masomo utanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021.

02. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

2:1. SARE ZA SHULE:

(A) WAVULANA:

- (i) Suruali mbili ya kaki na kijani jeshi (angalia sample).
- (ii) Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi.
- (iii) Viatu vyeusi na soksi nyeupe.
- (iv) Sweta rangi ya blue.

(B) WASICHANA:

- (i) Sketi mbili ndefu za rangi ya kaki na kijani jeshi (angalia sample).
- (ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi.
- (iii) Viatu nyeusi (flat shoes) na soksi nyeupe.
- (iv) Sweta rangi ya blue.

2:2. VIFAA VYA MICHEZO:

- (i) Bukta.
- (ii) Raba jozi moja.
- (iii) Fulana (T-shirt)rangi nyeupe, nyekundu yenye mikono mifupi.
- (iv) Soksi jozi mbili ziwe ndefu.
- (v) Track suit nyekundu.

2:3. VIFAA VYA MASOMO:

Unatakiwa kuja na vifaa vya masomo kama ifuatavyo:

- Madaftari makubwa (counter book) kumi na mbili (2&3 quires).
- Peni, penseli, faili la kuhifadhia taarifa za mwanafunzi.
- Mkebe (mathematical set)
- Four Figure.

03. MAAGIZO MENGINE:

Kutakuwa na kikao cha wazazi mara tu baada ya kufungua shule, kwa ajiri ya kujadili chakula cha wanafunzi shuleni.

NB:Siku ya kuripoti hakikisha mwanafunzi anafika kuripoti na Mzazi/Mlezi wake.

KARIBUNI SANA BUJELA SEKONDARI IMETOLEWA NA:

.....

ISSA SALUM NYENJE

MKUU WA SHULE